Ushauri wa COVID-19 kwa familia

Ilisasishwa Juni 2021

Tunafanya kazi kwa karibu na KamatiKuu ya Ulinzi wa Afya ya Australia (Australian Health Protection Principal Committee (AHPPC)), Idara ya Afya ya NSW na mashirika mengine kuhakisha shule zetu ziendelee kuendesha kwa njia za salama zaidi ziwezekanavyo katika mazingira ya COVID-19.

Ushauri uliosasishwa kutoka Idara ya Afya ya NSW

Habari za sasisho kuhusu COVID-19 zinatolewa kila mara. Familia zinahimizwa kufuatilia tovuti ifuatayo kwa habari za hivi karibuni tovuti ya Serikali ya NSW (NSW Government website).

Katika tukio la amri ya kukaa nyumbani kutumiwa na Idara ya Afya ya NSW kwa sababu kuzuka kwa COVID-19 kunaweza kuwa na mabadiliko katika shughuli za shule. Tafadhali uliza shule yako juu ya mabadiliko ya shughuli na fuata ushauri wote unaopewa na wafanyakazi wa shule yako, ikiwemo kutoingia viwanja vya shule kwa madhumuni yasiyo ya muhimu ikiwa itaombwa.

Kujifunza kutoka nyumbani

Wanafunzi watasaidiwa kujifunza kutoka nyumbani katika hali zifuatazo:

- Ikiwa wanatakiwa kujitenga kwa sababu ya kuwa mtu wa karibu wa kesi chanya au inayoshukiwa ya ugonjwa wa COVID-19.
- Ambapo shule hiyo inaelekezwa chini ya ushauri wa afya ya umma ili kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya kujifunza pale pale shuleni kwa watoto wa wafanyakazi wa lazima kutokana na mlipuko wa COVID-19.

Kujifunza kutoka nyumbani kunaweza kuwa aina nyingi, ikiwemo rasilimali za mtandaoni na nje ya mtandao na vifaa vilivyochapishwa kama vile karatasi za kazi na nyenzo.

Ushauri wa mahudhurio wakati wa kujifunza pale shuleni

Kwa mujibu wa ushauri kutoka Idara ya Afya ya NSW, wazazi na walezi wanakumbushwa **WASIPELEKE** watoto shuleni kama hao ni wagonjwa, hata kama wana dalili ndogo zinaofanana za mafua.

Idara ya Afya ya NSW imeomba kuwa shule zimhimize yeyote ambaye ni mgonjwa au ana dalili ndogo sawa na homa (flu), kupanga kupimwa kupitia daktari wao wa eneo ama mojawapo ya kliniki za COVID-19 (COVID-19 clinics).

Wanafunzi na wafanyakazi ambao wana dalili zinazofanana mafua (flu) wanapaswa kupimwa na kutoa nakala ya jibu hasi la kipimo cha COVID-19 na kuwa bila dalili kabla kuruhusiwa kurudi shuleni.

Wanafunzi ambao hawapati kipimo cha COVID-19 hawataruhusiwa kurudi shuleni kwa kipindi cha siku 10. Kuongeza, lazima wawe hawana dalili kwa angalau siku 3 kabla ya kurudi shuleni.

Ushauri wa mahudhurio wakati wa kujifunza pale shuleni (inayoendelea)

Wanafunzi ambao wana rhinitis ya mzio wa msimu au hali nyingine inayoonekana sawa na dalili za homa (flu) wanapaswa bado kupimwa COVID-19 na kurudi na majibu hasi la kipimo. Wakati dalili zao zinadumuisha zaidi ya siku 10, wanafunzi wanapaswa kutoa hati ya maandishi kutoka daktari wao kuthibitisha dalili ni kawaida kwa hali yao. Ikiwa mwanafunzi huyo anapata dalili mpya au zilizobadilika, anapaswa kupimwa kwa COVID-19. Pata habari zaidi juu ya dalili za COVID-19 (COVID-19 symptoms).

Kupimwa kwa COVID-19 kwa wanafunzi walio afya ngumu au ulemavu inaweza kuwa changamoto. Katika hali hizi, shule zitaomba mzazi au mlezi atathmini mtoto wake kwa daktari wake. Wakati daktari anaamua kwamba kipimo cha COVID-19 hauhitajiki, nyaraka lazima zipewe shule ili kuthibitisha kuwa mwanafunzi hana dalili ambazo zinahakikisha kipimo cha COVID-19. Cheti lazima pia ionyeshe kuwa mwanafunzi anaweza kurudi shuleni.

Ukumbusho kwa shule zote na familia zote

Ni muhimu kwa shule na familia ziendelee kufuata miongozo ya COVID-19. Hasa tunataka kuonyesha zifuatazo:

- Shule zinapaswa kuendelea:
  - kutekeleza usafi wa binafsi, kukaa mbali wa kimwili, kusafisha na utunzaji wa kumbukumbu.
  - inapowezekana, tumia maeneo ya nje kama hali ya hewa ni sawa, au nafasi kubwa wazi ili kuwezesha umbali kwa kutosha wa mwili.
  - kuhakikisha kuwa wageni wote kwa mahali pa shule ni wazima na bila dalili, wanafuata mipangilio ya kuingia ikiwemo kukubali kwamba watafuata mahitaji ya COVID-19 kwa wageni, wakandarasi na watoaji wa huduma kila wakati wanapotembelea. Wageni wote wanapaswa pia kuingia kwa kutumia Service NSW QR code. Wazazi na walezi ambao wanaacha au kuchukua wanafunzi hawahitaji kuingia au kutumia Service NSW QR code.

Kuvaa barakoa (mask) za uso na uchunguzi wa joto

Mtu yeyote anayetaka kuvaa barakoa (mask) yake shuleni hatazuia kufanya hivyo.

Wakati wa vipindi ambapo Amri za Afya ya Umma zimeamriwa kuvaa barakoa (mask) za uso katika usafiri wa umma, wanafunzi wenye umri wa miaka 13 na zaidi wanapaswa kufuata elekezo hili. Wafanyakazi wanapaswa pia kufuata elekezo hili wakati wanaposafiri katika usafiri wa umma pamoja na wakati wa safari katika usafiri wa umma au kwa huduma ya usafiri wa kukodi au wa kibinafsi.

Uchunguzi wa joto ulioenea hautakiwa au kushauriliwa katika shule.

Usafishaji wa shule na bidhaa za usafi

Shule yako itaendelea kupokea usafishaji wa ziada kulingana na miongozo wa AHPPC na ushauri kutoka Idara ya Afya ya NSW. Maeneo muhimu yanajumuisha maeneo ya kuguswa sana na nyuso ngumu zingine, vipete vya milango, kabati za kufunga, swichi za mataa, papi za ngazi katika maeneo ya ngazi na ya harakati. Kutakuwa pia usafishaji wa ziada wa vyoo na vifaa vya maji ya kunywa na kuongeza vifaa kama sabuni.

Shule zitaendelea kutoa bidhaa za usafi zikiwemo sabuni ya maji, sanitaiza ya mikono, taulo za karatasi, dawa ya uso, vifuto vya dawa ya kuua vijidudu.

Kujibu kesi za COVID-19

Kuna mpango wazi uliopo kwa shule kujibu kwa wagonjwa wowote wa ugonjwa wa COVID-19 walioshukiwa au kuthibitishwa. Tunafanya kazi kwa karibu na Idara ya Afya ya NSW na tutawasiliana na wazazi ikiwa hali itatokea. Soma zaidi kuhusu itifaki yetu ya kujibu kwa kesi za COVID-19 (Response protocols for COVID-19 cases).

Usafiri

Huduma za basi kwenda na kutoka shule ziendelee kufanya kazi kama kawaida. Kupata ushauri wa usafiri kwenda na kutoka shule, rejea kwa Usafiri kwa NSW (Transport for NSW).

Huduma ya Wakalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi tafadhali upigie simu mkuu wa shule yako. Kama unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali pigia simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na omba kwa mkalimani katika lugha yako. Hutatozwa kwa huduma hii.